

**UUZAJI**
Serikali kufufua mpango wa kuhifadhi mavuno ya wakulima kwenye maghala
UK3




**MAENDELEO**
Wizara yazindua mradi wa mabilioni ya pesa kuteka maji ardhini katika maeneo kavu UK 3

**KILIMO**
UK kujenga kiwanda cha kutayarisha viazi kwa gharama ya Sh2.3b Elgeyo Marakwet




UK 4

www.mygov.go.ke

FEBRUARI 7, 2023

# MyGov.

TATHMINI YAKO YA WIKI

Toleo No. 30/2022-2023

## Watumishi wa umma waliostaafu kunufaika na mpango mpya wa bima

NA **ANITA OMWENGA** NA **FLORENCE KINYUA** (KNA)

Serikali hivi karibuni itatekeleza mpango wa bima ya matibabu baada ya kustaafu kwa watumishi wa umma ili kuwakinga dhidi ya kutumia marupurupu yao duni ya kustaafu kugharamia matibabu yao au kutegemea watoto wao.

Katibu wa Utumishi wa Umma Bw Amos Gathecha alisema kwamba utafiti kuhusu kuanzishwa kwa mpango huo wa baada ya kustaafu umekamilika na kuwasilishwa kwa Baraza la Mawaziri kuidhinishwa

"Tulipokea ripoti ya utafiti huo wiki mbili zilizopita na tunasubiri uidhinishwe," alisema akiwa Muranga katika hafla ya uhamasisho kuhusu mpango huo mkubwa wa bima ya matibabu ya watumishi wa umma ya mwaka wa kifedha wa 2022/2023 uliofanywa na Hazina ya Taifa ya Bima ya Afya (NHIF).



Katibu wa Utumishi wa Umma, Bw Amos Gathecha

Katibu alithibitisha kuwa Baraza la Mawaziri litakapoidhinisha ripoti hiyo ya utafiti, watumishi wa umma waliostaafu wataanza kuchangia bima yao ya matibabu wakistaafu.

"Lengo la mpango huu ni kuwapa heshima watumishi wetu wa umma hata wakistaafu kwa sababu zote tunajua mzigo wa maradhi ambao wengi wao wanakabiliana nao na wanalazimika kutegemea wasamaria wema kulipa hili zao za matibabu,"alisema.

Mpango huo utahakikisha kuwa watumishi wa umma wanaishi maisha ya heshima, kwa kuwa watumishi wengi wastaafu wa umma hawana bima ya afya.

Katibu alishauri watumishi wa umma kujifahamisha na manufaa yote wanayo-

ENDELEA UK 2

# Mikakati kupeleka vitabu vya kiada vya Gredi 7 katika shule

Afisa Mkuu Mtendaji wa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) Profesa Charles Ong'ondo anasema kwamba shehena ya seti tatu za vitabu hivyo tayari zimepelekwa shuleni

**NA CHRIS MAHANDARA (KNA)**

Serikali imeweka hatua kali za kuhakikisha nyenzo za masomo za Gredi 7 zimefika katika shule zote nchini.


Afisa Mkuu Mtendaji wa Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala Kenya (KICD) Profesa Charles Ong'ondo alisema kwamba shehena ya seti tatu za vitabu hivyo tayari zimepelekwa shuleni.

Profesa Ong'ondo alisema kwamba vitabu hivyo vya kiada kuhusu elimu ya afya, kilimo, na masomo ya mazoezi ya mwili kwa wakati huu vinapatiwa wanafunzi kote nchini, na akaongeza kuwa KICD kwa ushirikiano na maafisa wa Wizara ya Elimu, inafuatilia vitabu vilivyosalia kuhakikisha vitapelekwa shuleni kwa wakati.

Alisema kwamba masomo ya Sekondari Msingi yameanza vyema, na akaongeza kuwa mashirika yote yanayohusika yanaendelea kushughulikia changamoto zinazoibuka.

Alisema kwamba KICD, inafuatilia zoezi hilo. Alitangaza kwamba uchunguzi utafanywa Februari kutathmini nyenzo zaidi za masomo zinazohitajika kuwezesha mpito bila tatizo.

ENDELEA UK 2



**Afisa Mkuu Mtendaji wa Kenya Institute of Curriculun Development (KICD) Prof. Charles Ong'ondo, wakati wa usambazaji wa vitabu vya kiada vya sekondari msingi mjini Kisumu. Aliandamana na mwalimu mkuu wa Rabuor Primary School, Dickson Awuor. Picha na Chris Mahandara**




**Takwimu za Wiki**

**15B**
Idadi ya miti serikali inalenga kupanda kote nchini kufikia 2030

**4,000**
Kiasi cha pesa ambazo zimetengwa kuboresha miundomsingi katika taasisi za elimu

**20,000**
Ekari za ardhi ambazo National Irrigation Authority (NIA) itatumia kukuza mpunga

**52**
Idadi ya vituo vya Huduma ambavyo vipo nchini

**1966**
Mwaka ambapo MV Uhuru 1 ilijengwa kusafirisha mafuta Uganda na Tanzania

**100M**
Gharama ya kituo kipya cha mabasi kilichozinduliwa Narok mjini

" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"

HOMA · KIKOHOZI · KUSHINDWA KUPUMUA · MAUMIVU KOONI · KUUMWA NA KICHWA

# Watumishi wa umma waliostaafu kunufaika na mpango mpya wa bima



ENDELEA KUTOKA UK 1

paswa kupata chini ya NHIF. "Mpango huo wa matibabu unatoa manufaa zaidi kama yanayohusiana na kazi katika Sheria ya WIBA, bima ya maisha ya makundi na bima ya kibinafsi ya ajali katika kundi miongoni mwa zingine," alisema. Wakati huo huo, katibu ambaye alikuwa ameandamana na Kaimu Afisa Mkuu Mtendaji wa Huduma Kenya Mugambi Njeru, pia alikagua ubora wa utoaji huduma katika kituo cha Huduma cha Murang'a. Alipongeza wafanyakazi kwa kuendelea kutoa huduma kwa umma kwa kujitolea kwa bidii na kuzingatia Viwango vya Utoaji Huduma vya Huduma Kenya.

"Vituo vya Huduma sasa vimekuwa ofisi za kwanza na mwisho za serikali. Inatia moyo kuona umma ukitafuta huduma katika Vituo vya Huduma," aliongeza Katibu.

> Serikali inapanga kufanya huduma 5,000 kuwa za kidijitali kwa ushirikiano na WB-Gathecha

Alisema kwamba huku serikali ikipanga kufanya huduma 5000 za serikali kuwa za dijitali, wanazungumza na Benki ya Dunia kuongeza idadi ya Vituo vya Huduma nchini.

"Kwa wakati huu tuna vituo 52 vya Huduma na Mpango Mkuu wa Huduma unaendelea kutafuta njia za kuongeza idadi hadi 340 kufanikisha utoaji wa huduma," alisema

# Mikakati kupeleka vitabu vya kiada vya Gredi 7 katika shule za umma

ENDELEA KUTOKA UK 1

Aliomba wazazi ambao wamehamisha watoto wao hadi shule tofauti kuarifu ofisi za elimu ili kuhakikisha kila shule inapata vitabu vya kutosha.

Akizungumza katika shule ya msingi ya Migosi, Kisumu katika ziara ya ukaguzi, Profesa Ong'ondo alisema pesa za kufadhili masomo ya Sekondari Msingi tayari zimetumwa kwa akaunti za shule kuhakikisha mpito unafaulu bila vikwazo.

Hata hivyo alionya walimu dhidi ya kutoza ada zaidi akiwataka kujadiliana na wazazi na kukubaliana jinsi ya kununua sare na mahitaji mengine.

Kati ya Sh15,000 zilizotengewa kila mwanafunzi, alisema Sh4,000 zitakuwa za kuimarisha miundomsingi ya shule katika taasisi za masomo, na akaonya wakuu wa shule dhidi ya kuhamisha mzigo huo kwa wazazi.

"Tunapoanzisha mpango huu, serikali itakagua nyenzo hizi na kuona ikiwa pesa hizo zinafaa kuongezwa," alisema. Tume ya Huduma ya Walimu (TSC),



Afisa Mkuu Mtendaji wa Kenya Institute of Curriculum Development (KICD), Prof. Charles Ong'ondo.

alisema, inaendelea na mchakato wa kutuma walimu wa shule za sekondari ya msingi, na akahimiza wakuu husika kutathmini uhitimu na ujuzi wa walimu katika shule za msingi na kuruhusu wale waliohitimu kusaidia kufanikisha sekondari msingi.

Kwa masomo ya kiufundi, Profesa Ong'ondo alihimiza wakuu wa shule kuzuia na wale wa shule za sekondari kuu kuruhusu wanafunzi kutumia maabara na mafunzo ya kiufundi huku hatua za kunyoosha JSS zikiendelea.

Mkurugenzi wa Elimu katika kaunti ndogo ya Kisumu ya Kati , Charles Angiela, alisema kwamba shule 29 za umma na 41 za kibinafsi katika eneo hilo ziliidhinishwa kuwa na Sekondari Msingi. Aliongeza kuwa jumula ya wanafunzi 4,888 katika kaunti ndogo hiyo wanatarajiwa kujiunga na Sekondari Msingi na akaongeza kwamba kufikia sasa asilimia 70 wameripoti. Uchunguzi uliofanywa na ofisi yake, alisema, ulifichua kwamba zaidi ya walimu 30 wa shule za msingi katika eneo hilo wana digrii za Uzamili na wengine wengine wakiwa na digrii katika Elimu. Alisema kwamba hii ni ishara chanya kwamba sekondari ya msingi itafaulu.


NDMA

## MAMLAKA YA KITAIFA YA KUDHIBITI KIANGAZI

## MWALIKO WA WAKANDARASI KWA KAZI NDOGO

## NDMA/PRQ/15/2022-2024

Mamlaka ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukame (NDMA) ni shirika la umma lililoanzishwa na Sheria ya Mamlaka ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukame (NDMA), 2016. Hapo awali lilikuwa likifanya kazi chini ya Sheria ya Mashirika ya Kitaifa (Sura ya 446) ya Sheria za Kenya kwa Notisi ya Kisheria Nambari 171 ya Novemba. 24, 2011.

NDMA inaalika kampuni zinazostahiki sifa za awali za wakandarasi kwa kazi ambazo zinaweza kuwa zilizopatikana kutoka kwa tovuti yetu www.ndma.go.ke au kutoka kwa www.tenders.go.ke

Hati iliyokamilishwa ya zabuni inapaswa kuwasilishwa, katika bahasha zilizofungwa na nambari ya kumbukumbu ya zabuni na jina lililowekwa alama wazi juu, inapaswa kutumwa kwa:

**Afisa Mkuu Mtendaji**
**Mamlaka ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukame**
**Lonrho House, Standard Street, Orofa ya 8**
**P.O. Box 53547 - 00200, NAIROBI**

Hati hizo, katika bahasha zilizofungwa, zinapaswa kuwekwa kwenye sanduku la zabuni lililo katika Mapokezi ya NDMA, Orofa ya 8, Lonrho House, Barabara ya Standard, Nairobi, ili kupokelewa kabla au kabla ya **Februari 28, 2023 saa 10:30 asubuhi.** Hati zilizowasilishwa baada ya tarehe ya mwisho hazitakubaliwa.

Zabuni za kielektroniki hazitakubaliwa

Hati hizo zitafunguliwa mara moja baada ya hapo katika Ukumbi wa Mikutano kwenye Orofa ya 17, Lonrho House, Standard Street, Nairobi mbele ya Wazabuni au wawakilishi wao wanaochagua kuhudhuria.

**AFISA MKUU MTENDAJI**

KENYA VISION 2030



REPUBLIC OF KENYA

## MAMLAKA YA KUSTAWISHA MAJI YA TANATHI

TANATHI

## NAFASI ZA KAZI (MABADILIKO)

Mamlaka ya Kustawisha Maji ya Tanathi (TAWWDA) ni Shirika la Serikali chini ya Wizara ya Maji, Usafi na Unyunyizaji lililoundwa chini ya kifungu cha 65 cha Sheria ya Maji ya 2016 na kuanzishwa kupitia Nyongeza ya Gazeti la Kenya Na.59, Notisi ya Kisheria Na.28 ya tarehe 26 Aprili 2019. Mamlaka ni mojawapo ya Mashirika Tisa (9) ya Ustawishaji wa Maendeleo ya Maji yaliyoanzishwa kwa kufuata Katiba ya Kenya, 2010.

Kwa mujibu wa Sheria ya Maji ya mwaka 2016, jukumu la msingi la TAWWDA ni kuhakikisha uwajibikaji, ufanisi na utoaji wa maji kiuchumi katika kaunti nne (4) za Kitui, Machakos, Makueni na Kajiado.

Mamlaka inatarajia kuajiri watu wanaofaa na wenye sifa za kujaza nafasi zifuatazo ambazo wamiliki wake watakuwa Makao Makuu ya Mamlaka (Kitui).

| Jina la Kazi | Daraja | Namba ya Marejeleo | Idadi |
|---|---|---|---|
| Meneja, Mipango na Usanifu wa Miundombinu | TAWWDA 3 | ADVERT/TAWWDA/01/MIPD/2023 | 1 |
| Mhasibu Mwandamizi | TAWWDA 5 | ADVERT/TAWWDA/02/SA/2023 | 1 |
| Mhandisi Mwandamizi, Miundombinu Kupanga na Kubuni | TAWWDA 5 | ADVERT/TAWWDA/03/SE/2023 | 1 |
| Msimamizi Mkuu Msaidizi wa Ofisi | TAWWDA 6 | ADVERT/TAWWDA/04/PAOA/2023 | 1 |
| Dereva Mkuu | TAWWDA 7 | ADVERT/TAWWDA/05/PD/2023 | 1 |

Waombaji wanaovutiwa na wanaostahiki wanapaswa kuingia katika tovuti ya TAWDA www.tanathi.go.ke kwa mahitaji ya kina, sifa na maagizo ya jinsi ya kutuma maombi yao ya kazi.

Maombi yote yanapaswa kuwasilishwa kabla ya **Alhamisi tarehe 2 Machi, 2023 saa 5.00 jioni.**

Mamlaka ya Kustawisha Maji ya Tanathi ni mwajiri anayetoa fursa sawa. Wanawake, vijana, walio wachache, waliotengwa na watu wanaoishi na ulemavu wanahimizwa kutuma maombi.

Tutawasiliana tu na wagombea watakaoorodheshwa kupitia anwani walizoandika katika barua zao za maombi.

***Ombi la mgombea yeyote atakayepatikana akidanganya litafutiliwa mbali.***

KENYA VISION 2030

# Serikali kuimarisha mfumo wa risiti kwenye mabohari

NA KIPTANUI CHERONO (KNA)

Serikali imetangaza mipango ya kufufua Mfumo wa Risiti wa Mabohari (WRS) ili kusaidia wakulima kupunguza hasara baada ya mavuno.

Katibu wa Idara ya Serikali ya Biashara Alfred K'Ombudo alisema kwamba mfumo huo ni muhimu kwa juhudi za serikali za kuimarisha uzalishaji.

Akizungumza alipozuru Uasin Gishu kukagua mabohari yaliyoidhinishwa, Katibu alisema kwamba kutia nguvu WRS kutahakikisha wakulima wanapata vituo bora vya uhifadhi ambavyo vitasaidia kupunguza hasara baada ya mavuno.

"Tunataka kuwa na mazungumzo na taasisi kama Bodi ya Taifa ya Nafaka na Mazao (NCPB) na wadau wengine kupanua huduma kwa wakulima kupitia mabohari yaliyoidhinishwa yanayohakikishia wakulima uhifadhi salama wa nafaka yao, ufikishaji salama sokoni na upatikanaji wa bidhaa za kifedha kwa kutumia wanachohifadhi katika maghala," alisema



Katibu wa Biashara Alfred K'Ombudo akiandamana na Kamishna wa Kaunti ya Uasin Gishu Dkt Eddyson Nyale, mshirikishi wa NCPB eneo la North Rift Gilbert Rotich (pembeni kushoto).

Katibu akiwa katika depo ya Eldoret ya NCPB.

"Kwa kutumia Mfumo wa Risiti wa Mabohari, ambao tunatazamia kutia nguvu, kutawezesha wakulima kupata usaidizi wa kifedha mapema iwezekanavyo wakisubiri bei bora; mfumo huo pia utatoa hifadhi salama," alisema K'Ombudo.Katibu alisema kwamba serikali itaungana na wadau kadhaa kuongeza idadi ya mabohari yanayotoa WRS. "Tunataka kupanua upatikanaji wa mabohari yaliyoidhinishwa kwa WRS kote nchini na kuwapa wakulima huduma hiyo kwa wingi zaidi," alisema.

Alisema kwamba uhifadhi salama wa nafaka katika mabohari yaliyoidhinishwa unasababisha upatikanaji bora wa soko na upatikanaji wa unga bora na bidhaa zingine. Katibu pia akitembelea chama cha Ushirika cha Wakulima cha Mateeny Soy, alipohimiza wakulima kuunda na kujiunga na vyama vya ushirika ili wanufaike na pembejeo nafuu za kilimo na bei bora za zao lao.

# Wizara yazindua mradi wa mabilioni wa maji ya chini ya ardhi kaunti kame

NA BERNADETTE OWADE (PCO)

Wizara ya Maji, Usafi na Unyunyuzaji itatekeleza mradi wa Sh15.5 bilioni uliofadhiliwa na Benki ya Dunia wa Ustahimilivu wa Maji ya Chini ya Ardhi katika kaunti tano kame na nusu kame (ASAL) ili kutatua uhaba wa bidhaa hiyo katika maeneo hayo

Akizungumza kwenye hafla ya kuzindua mradi huo unaoitwa Mradi wa ustahimilivu wa maji ya chini ya ardhi katika upembe wa Afrika (HoAGW4RP katika hoteli ya Nairobi, Waziri wa maji Alice Wahome alisema kwamba lengo kuu la mradi huo ni kuongeza upatikanaji na usimamizi wa maji ya chini ya ardhi katika maeneo ya Upembe wa Afrika. Bi Wahome alifichua kwamba kaunti zinazolengwa na Turkana, Marsabit, Mandera, Wajir na Garissa ambapo watu wapatao 1.5 milioni maeneo ya mashambani watanufaika na mradi huo. "Mradi huu unahusu ukarabati, ujenzi na usimamizi endelevu wa visima na pia kurudisha, kuongeza na kuimarisha




Waziri wa maji Alice Wahome

shughuli za uhifadhi wa maji," alisema Waziri. Bi Wahome aliongeza kuwa mradi huo utawezesha watakaonufaika kupata usambazaji wa maji ulioimarika, ujenzi wa vituo vipya vya maji na kukarabati vilivyomo na kuwezesha taasisi za maji ya chini ya ardhi kupata habari muhimu za usimamizi wa maji ya chini ya ardhi. Mpango wa Ustahimilivu wa Maji ya Chini ya Ardhi katika ukanda wa Upembe wa Afrika (HoAGW4RP) ni mpango unaoshirikisha Kenya, Somalia, Ethiopia, South Sudan, Djibouti, Eritrea na IGAD.

Hafla hiyo ya kuzindua mradi huo ulihudhuriwa na magavana Mohamed Adan Khalif (Mandera), Ahmed Abdullahi (Wajir), Nathif Jama (Garissa), Mohamud Mohamed Ali (Marsabit),Jeremiah Lomorukai (Turkana), na mwakilishi wa Benki ya Dunia. Waziri alitambua jukumu muhimu linalotekelezwa na Benki ya Dunia kwa kufadhili mradi huo kupitia mkopo wa dola 135 Milioni (Sh15.5 bilioni) ambazo zitatolewa kwa kipindi cha miaka sita kutoka 2022 hadi 2027.

KDC KENYA DEVELOPMENT CORPORATION

## ONYESHO LA NIA (EOI)

## USHAURI WA UTOAJI WA HUDUMA ZA USHAURI WA MUAMALA

Shirika la Kusimamia Maendeleo Kenya (KDC) ni Shirika la Serikali lililoanzishwa ili kuwezesha Maendeleo ya Viwanda na Kiuchumi nchini Kenya kwa Kuanzisha, Usaidizi au Upanuzi wa Viwanda, Biashara na Biashara zingine.

Jukumu la KDC ni kukuza maendeleo endelevu ya kiuchumi kwa kutoa fedha za maendeleo, fedha za miundombinu, usaidizi wa biashara na huduma za ushauri kwa viwanda vya kati na vikubwa, miradi ya miundombinu na shughuli za kibiashara katika sekta zinazolengwa nchini Kenya na kwingineko.

Shirika linaalika kampuni zinazostahiki na zilizohitimu kwa **Onyesho la Nia (EOI)- Ushauri wa Utoaji wa Huduma za Ushauri wa Muamala.**

Waombaji wanaostahiki wanaovutiwa wanaweza kupata hati za Onyesho la Nia (EOI) kutoka kwa Tovuti yetu www.kdc.go.ke au Tovuti ya Taarifa ya Ununuzi wa Umma katika https://tenders.go.ke/.

Waombaji wote wanaopakua hati ya EOI lazima wajisajili na Afisi ya Mfumo wa Usambazaji kwa kutuma barua pepe kwa: supplychain@kdc.go.ke

Hati za pendekezo zilizokamilishwa zitatiwa kwenye bahasha iliyofungwa iliyoandikwa kwa uwazi ***"EOI/KDC/040/2022-2023 Onyesho la Nia (EOI) - Ushauri wa Utoaji wa Huduma za Ushauri wa Muamala"*** na kutumwa kwa: -

**Mkurugenzi Mkuu**
**Shirika la Kusimamia Maendeleo Kenya (KDC)**
**Orofa ya 17, Uchumi House, Aga Khan Walk**
**P.O. Box 12665-00100, Nairobi**

Hati zilizokamilishwa zitawekwa kwenye kisanduku cha Zabuni kilicho katika eneo la Mapokezi kwenye Orofa ya 17, Uchumi House Aga Khan Walk, Nairobi, ili kupokelewa saa 10.00 asubuhi, Ijumaa tarehe 17 Februari 2023 au kabla. Hati za EOI zitafunguliwa mara moja baada ya hapo kwenye Mapokezi ya Orofa ya 17 mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kushuhudia.

**MKURUGENZI MKUU**
**SHIRIKA LA KUSIMAMIA MAENDELEO KENYA**

KENYA VISION 2030

## USAID AMPATH Uzima

MTRH

**Telephone: (+254)532033471/2 | Postal Address: P.O. Box 4606-30100, Eldoret, Kenya | Email: info@usaidampathuzima.or.ke**

## TENDER NOTICE

USAID AMPATH UZIMA, a Program managed by Moi Teaching and Referral Hospital (MTRH) and funded by USAID invites sealed bids for under listed.

**OPEN NATIONAL TENDERS**

| No | TENDER NO. | TENDER DESCRIPTION | ELIGIBILITY | CLOSING DATE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MTRH/T/101/2022-2023 | Supply, Delivery, Installation, Testing and Commissioning of Generator, Changeover Switch & Fuel Pump. | Open | 23rd February 2023 |
| 2. | MTRH/T/103/2022-2023 | Supply, Delivery, Installation, Testing and Commissioning of Automatic Voltage Regulator (AVR). | Open | 23rd February 2023 |

Complete set of Tender documents shall be obtained by interested Bidders free of charge from MTRH official website: **www.mtrh.go.ke** state tender portal: **https/supplier.treasury.go.ke publication.**

Tender bids in plain sealed envelopes bearing the Tender number ***(in bold)*** on the top right hand corner but with no indication of the Tenderer's name should be placed in the **Tender Box "B"** situated on the second Floor Left wing of the Main building of Moi Teaching and Referral Hospital ***(MTRH)*** or Posted to

**The Chief Executive Officer**
**Moi Teaching and Referral Hospital**
**P.O. Box 3-30100**
**ELDORET**

So as to be received on or before **Thursday 23rd February 2023, 10.00 am**. Bids will be opened publicly immediately thereafter in the presence of Bidders or their representatives who choose to attend at AMPATH Centre 1st Floor ATI Hall RM 118. Late bids will not be accepted whatsoever and shall be returned unopened.

Companies owned by Youth, Women and Persons with Disabilities are encouraged to participate. ***All queries regarding this tender should be directed to the Supply Chain Manager- AMPATHPlus.***

**CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**MOI TEACHING AND REFERRAL HOSPITAL**

KENYA VISION 2030

KOMESHA COVID-19
" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"
HOMA
KIKOHOZI
KUSHINDWA KUPUMUA
MAUMIVU KOONI
KUUMWA NA KICHWA

# Uingereza kujenga kiwanda cha kutayarisha viazi kwa gharama ya Sh2.3b Iten

NA ALICE WANJIRU (KNA)

Serikali ya Uingereza itajenga kiwanda cha kutengeneza viazi mbatata kitakachogharimu Sh2.3 bilioni mjini Iten, kaunti ya , Elgeyo Marakwet.

Akizungumza katika ofisi ya gavana katika hafla ya uzinduzi wa kiwanda hicho, Balozi wa Uingereza nchini Kenya, Jane Marriot alisema kwamba kiwanda hicho cha tani 60,000 ambacho kitakuwa kikitengeneza viazi mbatata na viazi vitamu kutahakikisha bei nzuri kwa wakulima wa mashamba madogo zaidi ya 10,000 katika kaunti hiyo na kanda kwa jumula. Balozi alisema kwamba kiwanda hicho kitaunda nafasi za kazi 5,000 moja kwa moja katika mwaka wake wa kwanza kikianza shughuli, ambazo zitaongezeka hadi 10,000 katika kipindi cha miaka mitano, zaidi ya kutoa aina mpya ya mbegu iliyo na uwezo wa kuongeza maradufu mavuno ya wakulima. "Kiwanda hicho, ambacho ni cha kwanza cha kutengeneza viazi katika eneo hilo, kitapunguza hasara baada ya mavuno na kutoa soko tayari la viazi, na kuhakikisha bei thabiti kwa zaidi ya wakulima wadogo 10,000 wa viazi katika kaunti ya Elgeyo Marakwet na katika kanda hii, na hivyo basi kubadilisha maisha ya maelfu ya wakulima hawa," alisema. Aliongeza kuwa kiwanda hicho kitainua vyama vya ushirika vilivyoko na vya zamani kwa kutoa mafunzo na kujenga uwezo wa wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo. Akisema kwamba wakulima wa mashamba madogo wameathiriwa na majadiliko ya hali ya hewa, uvamizi wa wadudu na ukosefu wa bei thabiti za zao lao, Balozi huyo alisema kwamba mradi huo utajenga ustahilimivu wao na kuwapa mapato thabiti ili familia ziweze kutumia ikiwemo kulipia karo wanafunzi wao.




Balozi wa Uingereza Kenya, Jane Marriott na Gavana wa Elgeyo Marakwet Wesley Rotich (kati). Serikali ya Uingereza itajenga kiwanda cha kutayarisha viazi mjini Iten kwa gharama ya Sh2.3 bilioni.

> Kiwanda kitapunguza hasara ya mavuno na kuwezesha viazi kununuliwa-Jane

Kiwanda hicho, ambacho ni ushirikiano wa serikali ya Uingereza na Select Fresh Produce Kenya Limited kitajengwa kupitia mpango wa Uingereza wa Maendeleo Endelevu ya Uchumi Mijini (SUED) kwa ushirikiano na Manispaa ya Iten. Gavana wa kaunti hiyo, Wisley Rotich alisema kwamba kaunti inaunga kikamilifu mradi huo, akisema wakulima wamekuwa wakifyonzwa na mawakala kwa kukosa mfumo wa uongezaji thamani. "Kaunti yetu ni ya pili kwa uzalishaji wa viazi nchini baada ya Nyandarua lakini wakulima hawana chochote cha kujivunia kutokana na jasho lao kwa kuwa pesa nyingi huenda kwa mabroka," alisikitika.

Gavana huyo alisema ametuma maafisa wa ushirika katika kila wadi kutia nguvu vyama vya ushirika akisema wakulima watatia saini kandarasi kama makundi na sio watu binafsi.

Afisa Mkuu Mtendaji wa Select Fresh Produce Kenya Eunice Mutua, alisema kwamba kiwanda hicho kitafanya kazi kwa karibu na wakulima wa eneo hilo kuhakikisha kwamba wanachozalisha kinatimiza viwango vya kimataifa kwa kuhakikisha wanatumia mbinu salama kwa mazingira na kuinua ustahilimivu wa mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema kwamba kiwanda hicho kitakuwa cha kwanza nchini na Cha tatu Afrika Kusini kutengeneza viazi mbatata na vitamu kwa soko la Ulaya.

REPUBLIC OF KENYA
nhc

## TENDER NOTICE

National Housing Corporation (N.H.C) invites sealed bids from eligible bidders for the following tenders;

| Tender Number | Tender Description | Closing Date & Time |
|---|---|---|
| NHC/TECH/KNYR/011/2022-23 | Proposed Kisumu Kanyakwar Phase III | 15th February 2023 at 11.00a.m |
| NHC/TECH/ELD/012/2022-23 | Proposed Eldoret Regional Office | 16th February 2023 at 11.00a.m |
| NHC/TECH/KRG/017/2022-23 | Proposed Kirinyaga Affordable Housing Project; Phase I; Sector A - Kirinyaga County. | 17th February 2023 at 11.00a.m |
| NHC/TECH/EMB/016/2022-23 | Proposed Embu Affordable Housing Project; Phase I; Sector A - Embu County. | 20th February 2023 at 11.00a.m |
| NHC/TECH/BIM/018/2022-23 | Supply, Installation, Configuration, and Commissioning of a Building Information Modeling (BIM) System | 21st February 2023 at 11.00a.m |
| NHC/ICT/019/2022-23 | Supply, Installation, Configuration, and Commissioning of a Push Notification System | 22nd February 2023 at 11.00a.m |
| NHC/SGS/020/2022-23 | Provision of Security and Guarding Services at NHC Properties | 24th February 2023 at 11.00a.m |

Tender documents can be downloaded ***free of charge*** from N.H.C website **www.nhckenya.go.ke** or **www.tenders.go.ke.** Enquiries can be made via email address: **info@nhckenya.go.ke.**

***Any addenda/additional information on the tenders will be posted on the N.H.C website.***

Duly completed bid documents shall be submitted in plain sealed envelopes clearly marked with the ***"Tender Number"*** and ***"Tender Description"*** and addressed to:-

**MANAGING DIRECTOR,**
**P. O. BOX 30257 – 00100,**
**NAIROBI.**

And be deposited in the Tender Box located on Ground Floor of N.H.C house, so as to be received on or before **the above indicated dates** and shall be valid for a period of 150 days after bid submission. Bids will be opened immediately thereafter in the presence of bidders and/or their representatives who choose to attend in the Conference Room located on 10th Floor of N.H.C House. **Late bids will be rejected.**

**Managing Director**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA
OFFICE OF THE REGISTRAR OF POLITICAL PARTIES
ORPP
Strengthening political parties

## TANGAZO LA NAFAZI ZILIZO WAZI KATIKA AFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA KISIASA (ORPP)

Afisi ya Msajili wa Vyama vya Kisiasa imebuniwa na Sheria ya Vyama vya Kisiasa, 2011 kama Afisi huru ya Serikali kwa maana ya Kifungu cha 260 cha Katiba ya Kenya, 2010. Mamlaka ya Afisi hiyo ni kusajili, kudhibiti, kusimamia Vyama vya Kisiasa. na kusimamia Mfuko wa Vyama vya Siasa.

Afisi inakaribisha maombi kutoka kwa waombaji waliohitimu ipasavyo kujaza nafasi zifuatazo zilizoachwa wazi katika uanzishwaji wake.

| NO. | JINA LA KAZI | GREDI | IDADI | NAMBA YA TANGAZO | MFUMO WA UAJIRI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Meneja, Fedha | 4 | 1 | RPP/1/2023 | Pensheni |
| 2. | Afisa wa Utawala | 6 | 1 | RPP/2/2023 | Pensheni |
| 3. | Msimamizi wa Ofisi | 6 | 1 | RPP/3/2023 | Pensheni |
| 4. | Mhasibu | 6 | 3 | RPP/4/2023 | Pensheni |
| 5. | Maafisa wa Usajili (Huduma za Nyanjani) | 6 | 4 | RPP/5/2023 | Pensheni |
| 6. | Afisa wa Uzingatiaji (Huduma za Nyanjani) | 6 | 3 | RPP/6/2023 | Pensheni |
| 7. | Afisa wa Kusimamia Rekodi **(Imetangazwa tena)** | 6 | 1 | RPP/7/2023 | Pensheni |
| 8. | Afisa wa Ushirikiano na Mahusiano | 6 | 1 | RPP/8/2023 | Pensheni |
| 9. | Afisa Karani | 8 | 8 | RPP/9/2023 | Pensheni |
| 10. | Dereva | 9 | 2 | RPP/10/2023 | Pensheni |
| 11. | Wafanyakazi Wasaidizi | 10 | 1 | RPP/11/2023 | Pensheni |

Maelezo ya kina na ya kina ya kazi na mahitaji ya nafasi hizo hapo juu yanapatikana katika tovuti ya ORPP: **www.orpp.or.ke**

**Jinsi ya Kutuma Maombi**;

1. Watu wanaovutiwa na wenye sifa wanaombwa kutuma maombi yao kwa kujaza nakala mbili za fomu ya maombi ya kazi ya ORPP. Fomu ya maombi inaweza kupakuliwa kutoka kwa tovuti ya ORPP, **www.orpp.or.ke**
2. Waombaji wanatakiwa kuwasilisha maombi yao pamoja na nakala ya Kitambulisho cha Taifa/Pasipoti, nakala za vyeti vya taaluma, ushuhuda na nyaraka nyinginezo muhimu ili wafike Ofisini kabla au kabla ya **tarehe 28 Februari, 2023**
3. Maombi yatumwe kwa:

   **Msajili wa Vyama vya Kisiasa**
   **Lion Place, Orofa ya 1 na ya 4**
   **Karuna Close, Waiyaki Way, Westlands**
   **P. O. Box 1131-00606 NAIROBI**
4. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni mwajiri wa fursa sawa. Watu wanaoishi na ulemavu wanahimizwa kutuma maombi.
5. Tutawasiliana na watu watakaoorodheshwa pekee. Ombi la yeyote atakayepatikana akidanganya litafutiliwa mbali.

ORPPKenya ORPPKenya www.orpp.or.ke @ORPPKenya KENYA VISION 2030






REPUBLIC OF KENYA

## BARAZA LA MAAFISA WA AFYA UMMA NA MAFUNDI

## MWALIKO WA ZABUNI

### ZABUNI YA USAMBAZAJI WA BIDHAA NA UTOAJI WA HUDUMA

1. Baraza la Maafisa wa Afya wa Umma na Mafundi linakaribisha Zabuni zilizofungwa kutoka kwa Wasambazaji kwa Usambazaji na Uwasilishaji wa aina zifuatazo:

| S/NO | NAMBARI YA KITENGO | MAELEZO | UHITIMU |
|---|---|---|---|
| **Usambazaji wa Bidhaa** | | | |
| 1. | PHOTC/ONT/PREQ/001/2022-2024 | Zabuni ya Usambazaji na Uwasilishaji wa Samani za Ofisi na Viunga | WAZI |
| 2. | PHOTC/ONT/PREQ/002/2022-2024 | Zabuni ya Usambazaji na Uwasilishaji wa Sare za Wafanyakazi na bidhaa zenye Chapa | AGPO |
| 3. | PHOTC/ONT/PREQ/003/2022-2024 | Zabuni ya Usambazaji wa Magazeti na majarida | AGPO |
| 4. | PHOTC/ONT/PREQ/004/2022-2024 | Zabuni ya Usambazaji wa Vifaa vya Ofisi ya ICT | WAZI |
| 5. | PHOTC/ONT/PREQ/005/2022-2024 | Zabuni ya udambazaji wa Matairi, Mirija na Betri | WAZI |
| 6. | PHOTC/ONT/PREQ/006/2022-2024 | Zabuni ya usambazaji na Uwasilishaji wa Vifaa na Vifaa vya Ofisi ya Jumla | AGPO |
| 7. | PHOTC/ONT/PREQ/007/2022-2024 | Zabuni ya usambazaji na Uwasilishaji wa Vifaa vya Kutumika vya Kompyuta | AGPO |
| 8. | PHOTC/ONT/PREQ/008/2022-2024 | Usambazaji wa maji ya kunywa ya chupa na vikombe vinavyoweza kutumika | AGPO |
| 9. | PHOTC/ONT/PREQ/009/2022-2024 | Usambazaji na utoaji wa maziwa, sukari na vinywaji mbalimbali | AGPO |
| 10. | PHOTC/ONT/PREQ/010/2022-2024 | Usambazaji na utoaji wa huduma za muda wa maongezi | AGPO |
| 11. | PHOTC/ONT/PREQ/011/2022-2024 | Usambazaji na uwasilishaji wa vyoo | AGPO |
| 12. | PHOTC/ONT/PREQ/012/2022-2024 | Usambazaji na utoaji wa vifaa vya uchunguzi na vielelezo | WAZI |
| 13. | PHOTC/ONT/PREQ/013/2022-2024 | Kubuni, uchapishaji na utoaji wa vyeti vya kitaaluma na kadi za index | WAZI |
| 14. | PHOTC/ONT/PREQ/014/2022-2024 | Usambazaji na utoaji wa vifaa vya kusafisha na sabuni | AGPO |
| **Utoaji wa Huduma** | | | |
| 15. | PHOTC/ONT/PREQ/016/2022-2024 | Zabuni ya Utoaji wa Huduma za Uchapishaji | WAZI |
| 16. | PHOTC/ONT/PREQ/017/2022-2024 | Utoaji Huduma za Usafiri na Tikiti za Ndege - ***(Kampuni zilizosajiliwa za IATA/KATA pekee)*** | WAZI |
| 17. | PHOTC/ONT/PREQ/018/2022-2024 | Utoaji wa Huduma za Ukaguzi wa Ndani na Nje | WAZI |
| 18. | PHOTC/ONT/PREQ/019/2022-2024 | Uhitimu wa Matengenezo, Huduma na Matengenezo ya Fotokopi | WAZI |
| 19. | PHOTC/ONT/PREQ/020/2022-2024 | Uhitimu wa Matengenezo, Huduma na Matengenezo ya Kompyuta, Printa na UPS | AGPO |
| 20. | PHOTC/ONT/PREQ/021/2022-2024 | Zabuni ya Kusafisha Mapazia, Seti za Sofa na Samani za Ofisi | AGPO |
| 21. | PHOTC/ONT/PREQ/022/2022-2024 | Utoaji wa Huduma za Ushauri ***(Makampuni na Watu Binafsi)*** | WAZI |
| 22. | PHOTC/ONT/PREQ/023/2022-2024 | Zabuni ya Utoaji wa Vifaa vya Mikutano katika Kaunti zote 47 | WAZI |
| 23. | PHOTC/ONT/PREQ/024/2022-2024 | Utoaji wa muundo wa wavuti, matengenezo na huduma za mtandaoni | AGPO |
| 24. | PHOTC/ONT/PREQ/025/2022-2024 | Utoaji wa huduma za upishi | WAZI |
| 25. | PHOTC/ONT/PREQ/026/2022-2024 | Utoaji wa huduma za muunganisho wa mtandao | AGPO |
| 26. | PHOTC/ONT/PREQ/027/2022-2024 | Barua pepe na huduma za mwenyeji wa Wavuti | WAZI |
| 27. | PHOTC/ONT/PREQ/028/2022-2024 | Utoaji wa bima ya matibabu kwa Wajumbe wa Baraza na watumishi | WAZI |
| 28. | PHOTC/ONT/PREQ/029/2022-2024 | Utoaji wa huduma za mahusiano ya umma | WAZI |

2. Utoaji wa zabuni utafanywa chini ya mbinu ya Utoaji Wazi kwa kutumia hati sanifu ya zabuni Zabuni iko wazi kwa Wazabuni wote waliohitimu na wanaopenda.
3. Mzabuni Aliyehitimu na aliyeorodheshwa anaweza kupata taarifa zaidi na kukagua Nyaraka za Zabuni wakati wa saa za kazi yaani saa 0900 hadi 1700 kwa anuani iliyotolewa kwenye hati ya zabuni.
4. Nyaraka za zabuni zinaweza kutazamwa na kupakuliwa bila malipo kutoka kwa tovuti **www.photc.org** Wazabuni wanaopakua hati ya zabuni lazima wapeleke taarifa zao mara moja kwa **photc.kenya@gmail.com / info@photc.org** ili kuwezesha ufafanuzi au nyongeza yoyote zaidi.
5. Zabuni zilizokamilishwa lazima ziwasilishwe kwa anwani iliyo hapa chini mnamo au kabla ya tarehe **21 Februari 2023 saa 12:30 mchana**. Zabuni za Kielektroniki hazitaruhusiwa.
6. Zabuni zitafunguliwa mara baada ya tarehe ya mwisho na muda uliotajwa hapo juu au tarehe ya mwisho na muda uliotajwa baadaye. Zabuni zitafunguliwa hadharani mbele ya wawakilishi wateule wa Wazabuni ambao wataamua kuhudhuria kwa anwani iliyotolewa kwenye hati ya zabuni.
7. Zabuni zilizochelewa zitakataliwa.

Serikali inahifadhi haki ya kukataa zabuni yoyote ikitoa sababu za kukataliwa na haijilazimishi kukubali zabuni ya chini kabisa au yoyote.

**MSAJILI/ CEO**
**BARAZA LA MAAFISA WA AFYA WA UMMA NA MAFUNDI**

KENYA VISION 2030

SPECIAL ECONOMIC ZONES AUTHORITY
"Powering Growth"

**UAP Old Mutual Tower, 14th Floor, Upper Hill Road**
**P.O Box 30418-00100, GPO**
**Nairobi, Kenya**
**Tel: +254 20 7863971**
**Email: info@sezauthority.go.ke**
**Website: www.sezauthority.go.ke**

## KAZI- AFISA MKUU MTENDAJI

Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZA) ni Shirika la Serikali chini ya Wizara ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda. Ilianzishwa kupitia Sheria ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi namba 16 ya mwaka 2015, kama taasisi. yenye jukumu la kuvutia, kuwezesha na kuhifadhi uwekezaji wa moja kwa moja wa ndani na nje ya nchi katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZs).

### REF. NO: - SEZA/CEO/01/2023

SEZA inataka kuajiri mtu mwenye uwezo, mwelekeo wa matokeo, ujuzi, mahiri, maono na uzoefu ili kujaza nafasi ya Afisa Mkuu Mtendaji (CEO) kwa mkataba wa miaka mitano(5) unaoweza kuongezwa mara moja kwa kuzingatia utendaji kazi unaoridhisha.

Majukumu makuu ya Afisa Mtendaji Mkuu ni pamoja na yafuatayo:
(i) Kutumikia kama Afisa Masuuli wa Mamlaka;
(ii) Kutekeleza na kuwasilisha mikakati, maamuzi na sera za Bodi;
(iii) Kuwa kiungo kati ya Bodi na Menejimenti;
(iv) Kutoa mawasiliano ya mara kwa mara, ya kina na ya haraka kwa Bodi kuhusu masuala muhimu ya kiufundi, kifedha na kiutawala;
(v) Kutoa ushauri kwa Katibu wa Baraza la Mawaziri anayehusika na Uwekezaji, Biashara na Viwanda kuhusu Masuala yanayohusiana na Kanda Maalum za Kiuchumi;
(vi) Kuratibu na kutekeleza Mpango Mkakati wa SEZA utakaotekeleza majukumu ya msingi ya Mamlaka;
(vii) Kutoa uongozi wa kimkakati, kuchora na kutekeleza mipango kwa ajili ya utekelezaji bora wa Mpango Mkakati wa Mamlaka;
(viii) Kuanzisha, kupitia na kusimamia utekelezaji wa sera na programu pamoja na kuoanisha taratibu za uendeshaji ili kuhakikisha udumishaji wa viwango vya juu vya utendaji na uwajibikaji;
(ix) Kuwajibika kwa utekelezaji wa Mkataba wa Utendaji Kazi;
(x) Kuanzisha na kudumisha ushirikiano na washirika wakuu wa kitaifa na kimataifa ili kukuza Uwekezaji;
(xi) Kusimamia na kudhibiti fedha na rasilimali nyinginezo za Mamlaka kwa ufanisi na kwa gharama nafuu kwa kushauriana na Bodi;
(xii) Kutambua na kuendeleza uwezo wa Mamlaka katika kuendesha programu kulingana na Mpango Mkakati ulioidhinishwa na Bodi;
(xiii) Kutayarisha mipango kazi ya mwaka na bajeti na kuwasilisha kwa Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa;
(xiv) Kufanya kazi nyingine zozote zitakazoagizwa na Bodi.

### Sifa za Kitaalamu na Uzoefu

Ili kuteuliwa katika nafasi hii mgombea lazima:
(i) Awe raia wa Kenya;
(ii) Awe na Shahada ya Kwanza katika mojawapo ya yafuatayo: Utawala wa Biashara, Uchumi, Fedha, utawala wa umma, Masoko, Usimamizi wa Kimkakati, Sheria au sayansi husika ya kijamii na kimwili na fani nyingine yoyote inayolingana nayo kutoka Chuo Kikuu kinachotambuliwa;
(iii) Awe na shahada ya uzamili katika mojawapo ya fani zifuatazo: Utawala wa Biashara, Uchumi, Fedha, utawala wa umma, Masoko, Usimamizi wa Kimkakati, Sheria au sayansi husika ya kijamii na kimwili na fani nyingine yoyote inayolingana nayo kutoka chuo kikuu kinachotambuliwa;
(iv) Awe na uzoefu wa kazi husika usiopungua miaka kumi na tano (15) ambapo miaka kumi (10) lazima awe katika ngazi ya uongozi wa juu wa taasisi ya umma au ya kibinafsi na kumi (10) katika uzoefu wa kuhitimu wa kuhudumu;
(v) Awe na ujuzi thabiti wa kukusanya rasilimali akiwa na washirika wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi.
(vi) Kuwa na ujuzi wa uongozi kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya kimkakati. Awe amechukua kozi ya Uongozi isiyopungua wiki sita (6) kutoka kwa taasisi inayotambulika;

### Umahiri Muhimu

(i) Awe na ujuzi mzuri wa mawasiliano ya mdomo na maandishi ikijumuisha uandishi wa ripoti;
(ii) Kuwa na uelewa mzuri wa Mamlaka ya SEZA;
(iii) Kuonyesha weledi na umahiri wa hali ya juu katika utendaji wa kazi;
(iv) Awe mwanachama wa chombo husika cha kitaaluma;
(v) Awe anajua kompyuta;
(vi) Kuwa na mahusiano mazuri ya kibinafsi, mazungumzo na sifa za juu za uongozi.

### Sura ya Sita ya Katiba

Waombaji waliofaulu watahitajika kukidhi masharti ya Sura ya sita ya Katiba ya Kenya 2010 kwa kuwasilisha vyeti vifuatavyo vya kufuata;
(i) Mamlaka ya Kukusanya Ushuru Kenya (Cheti cha Kuzingatia Ushuru);
(ii) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (Cheti cha Uzingatiaji);
(iii) Tume ya Elimu ya Vyuo Vikuu kwa digrii zinazopatikana nje ya Kenya;
(iv) Tume ya Maadili na Kupambana na Rushwa (Cheti cha Uzingatiaji);
(v) Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai (Cheti cha Maadili Bora);
(vi) Afisi ya Marejeo ya Mikopo (Cheti cha Uthibitisho)

### Malipo

Mgombea aliyefaulu atalipwa malipo mazuri yanayolingana na majukumu anayotekeleza

### Jinsi ya Kutuma Maombi

Waombaji waliohitimu wanapaswa kuwasilisha maombi yao ikiwa ni pamoja na barua ya kazi, wasifu kazi, nakala za vyeti vya taaluma na taaluma, vibali, ushuhuda, wadhamini watatu kupokelewa **Tarehe 23 Februari 2023** au kabla. Maombi yatumwe kwa barua pepe **chair@sezauthority.go.ke** au yawasilishwe kwa mkono kwa ofisi ya SEZA iliyoko kwenye Orofa ya 14, Jengo la UAP, Upper Hill.

Maombi yote yawe na alama ya wazi **"Maombi ya nafasi ya Afisa Mtendaji Mkuu"** na yatumwe kwa

**Mwenyekiti**
**Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Kiuchumi**
**UAP Old Mutual Tower, Orofa ya 14, Barabara ya Upper Hill**
**P.O Box 30418-00100, GPO**
**Nairobi, Kenya**

NB: Mamlaka ya Eneo Maalum la Kiuchumi imejitolea kutekeleza masharti ya Katiba - Kifungu cha 232 (1) kuhusu ushindani wa haki na sifa, uwakilishi wa jamii mbalimbali za Wakenya na kutoa fursa sawa za ajira kwa wanaume na wanawake, watu wa makabila yote na watu wenye ulemavu.

KENYA VISION 2030

KOMESHA COVID-19

" Virusi havitembei, watu huvisambaza, tukiacha kutembea, virusi vitakufa"




# Mswada kutatua masuala ya vijana wenye matatizo ya akili, jinsia mbili

**NA ANNE SABUNI (KNA)**

Serikali inatayarisha Mswada wa Maendeleo ya Vijana ambao utatatua masuala ya vijana, hasa walio na ulemavu wa akili na mwili na pia jinsia mbili.

Katika wa masuala ya vijana Ismail Maalim alisema kwamba Mswada wa Maendeleo ya Vijana unalenga kuinua heshima ya utu na kutobagua na pia utashughulikia mtoto mvulana na vijana walio na ulemavu ambao huwa wanapuuzwa wakati wa utungaji wa sera. Akizungumza akiwa Nakuru alipoongoza wataalamu kutayarisha Mswada huo mpya, Maalim alisema kwamba serikali inataka kuhakikisha vijana wote wanashughulikiwa katika mipango na miradi kwa pamoja. Akihimiza vijana kubadilisha mawazo yao na kuwajibikia maisha yao, Maalim alisema wako na nafasi nzuri ya kujishughulikia huku serikali ikisaidia juhudi zao kupitia sera na mipango ya kuwafanya wastawi. "Mtizamo kwamba ni serikali pekee inayoweza kuwafanya mfaulu lazima ubadilishwe. Jukumu ni lenu kuwajibikia maisha yenu kabla ya serikali kuingilia kati na kuweka mazingira bora," alisema. Mswada huo ambao tayari utafanikisha kupitishwa kwa Sheria ya Maendeleo ya Vijana Kenya itawapa vijana jukwaa la kuwezesha sauti zao kusikika huku wakishiriki katika siasa na shughuli zingine za uchumi.

"Vijana ni asilimia 75 ya watu wetu na hivyo lazima tuwashughulikie," alisema.


**Katibu wa Masuala ya Vijana, Ismail Maalim, ahutubia kundi la wataalamu kutoka Wizara ya Masuala ya Vijana ambao watashiriki kwenye shughuli ya wiki moja ya kubuni mswada wa ustawi wa vijana. Picha na Anne Sabuni**

nema
mazingira yetu | uhai wetu | wajibu wetu

# Mamlaka ya Kitaifa ya Kusimamia Mazingira

**Popo Road, off Mombasa Road P.O.BOX 67839-00200, Nairobi, Kenya,**
**Simu: 0724253398, 0735013046 B/Pepe: dgnema@nema.go.ke Tovuti: www.nema.go.ke**

## TAARIFA KWA UMMA KUTOA MAONI KUHUSU RIPOTI YA UTATHMINI WA ATHARI ZA MAZINGIRA KWA MRADI UNAOPENDEKEZWA WA NYUMBA NAFUU ZA HOMA BAY AWAMU YA 1 KWENYE PLOTI L.R. NAMBA MANISPAA YA HOMA BAY BLOCK 1/839 NDANI YA MANISPAA YA HOMA BAY KAUNTI YA HOMA BAY

Kwa mujibu wa Kanuni ya 21 ya Kanuni za Usimamizi na Uratibu wa Mazingira (Tathmini ya Athari na Ukaguzi), 2003, Mamlaka ya Kitaifa ya Usimamizi wa Mazingira (NEMA) imepokea Ripoti ya Utafiti wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa mradi uliopendekezwa hapo juu.
Mshauri, Shirika la Kitaifa la Ujenzi wa Nyumba, linapendekeza kuweka ujenzi wa nyumba za bei nafuu ambazo zitakuwa na jumla ya vitengo 400. Itakuwa na nyumba 120 aina ya Bedsitters(vitalu 4), nyumba 140 za chumba kimoja cha kulala (vitalu 7), nyumba140 za vyumba viwili vya kulala (vitalu 7) na vifaa vinavyohusika na vistawishi kwenye Ploti L.R. Nambari ya Homa Bay Municipality Block 1/839 ndani ya Manispaa ya Homa Bay ya Kaunti ya Homa Bay.

Zifuatazo ni athari zinazotarajiwa na hatua za kupunguza zinazopendekezwa:

| ATHARI | HATUA ZA KUPUNGUZA |
|---|---|
| Hatari ya Moto | • Ufungaji wa mfumo wa usalama wa moto - vifaa vya kuzima moto vinavyofaa, vituo vya kuunganisha reel ya hose na vidhibiti vya moto pamoja na mambo mengine kama lazima.<br>• Hifadhi ya maji ya kuzimia moto / tanki liwekwe mahali pake na lijazwe maji wakati wote |
| Upotevu wa viumbe hai | • Futa nyenzo zisizotumiwa kutoka kwenye tovuti mwishoni mwa awamu ya ujenzi ili kuruhusu upyaji wa mimea.<br>• Rejesha ardhi kwa njia ya mandhari ifaayo.<br>• Tumia hatua zinazofaa za kuhifadhi udongo ili kupunguza athari ya mmomonyoko. |
| Hatari ya uharibifu wa ardhi. | • Uchimbaji ufanyike mara moja kabla ya ujenzi badala ya kuacha udongo wazi kwa muda mrefu (miezi/miaka).<br>• Dhibiti mtiririko wa umakini na kukimbia ili kupunguza ujazo na kasi ya maji kutoka kwa maeneo ya kazi. |
| Kelele na uchafuzi wa mitetemo kupita kiasi. | • Wape wafanyakazi vifaa vinavyofaa na vya kutosha vya Kujikinga (PPEs)<br>• Hakikisha magari na mashine zote zinahudumiwa vyema.<br>• Epuka njia za ulipuaji wakati wa kusitisha isipokuwa ni lazima kabisa. |
| Usumbufu wa trafiki barabarani | • Wape wafanyakazi Vifaa vinavyofaa na vya kutosha vya Kujikinga (PPEs)<br>• Mkandarasi kuweka utaratibu wa kudhibiti kasi ya magari yanayosonga ili kupunguza utoaji wa vumbi<br>• Mwagilia maji mahali ambapo / inapohitajika angalau mara mbili kwa siku ili kupunguza uenezi wa vumbi.<br>• Mashine zinazotumiwa wakati wa ujenzi zitunzwe vya kutosha ili kupunguza utoaji wa moshi wa kutolea nje na uchafuzi wa mazingira. |
| Usalama na afya kazini | • Toa PPE zinazofaa kwa matumizi ya wafanyikazi na utekeleze matumizi yao.<br>• Toa vifaa vya kutosha vya huduma ya kwanza vilivyojaa kwenye tovuti na uteue wasaidizi wa kwanza waliofunzwa.<br>• Kuwa na rejista ya tukio/ajali kwenye tovuti ya ujenzi.<br>• Toa alama za dharura zinazofaa kwenye tovuti, taa za kutosha na vizuizi inapohitajika.<br>• Mkandarasi hupata bima ya WIBA kwa wafanyakazi wa ujenzi kwenye tovuti ya ujenzi.<br>• Muundo wa vitengo vya nyumba unapaswa kujumuisha sakafu ya kuzuia kuteleza na kuanguka.<br>• Kufanya kujenga uwezo na mafunzo kwa wafanyakazi/wafanyakazi kwa heshima ya Afya, Usalama na Mazingira Kazini. |
| Athari mbaya za kijamii. | • Kujenga ufahamu na uhamasishaji juu ya masuala ya VVU/UKIMWI na magonjwa ya zinaa.<br>• Kupitishwa na matumizi ya 'Nyumba Kumi' ndani ya mradi unaopendekezwa ili kuongeza mshikamano ndani ya mradi hasa wakati wa awamu ya uendeshaji wa mradi.<br>• Uundaji wa chama cha wakaazi kuandaa jamii ndani ya mradi uliopendekezwa ili kuelezea maswala ya kawaida ya wakaazi. |

| ATHARI | HATUA ZA KUPUNGUZA |
|---|---|
| Uchafuzi wa maji / uzalishaji wa taka za kioevu | • Hakuna kambi za ujenzi zitakazowekwa ndani ya mita 50 za njia ya mifereji ya maji na chanzo cha maji.<br>• Hifadhi zote za mafuta zinapaswa kuunganishwa ipasavyo.<br>• Kutoa vifaa vya udhu vya kutosha na vinavyofaa kwa mfanyakazi wa ujenzi.<br>• Majitaka yote yapitishwe na kuwekwa ndani ya mifumo ya usimamizi wa maji taka.<br>• Maji yanayotiririka usoni hayatachanganyika na maji machafu na yanapaswa kupitishwa ipasavyo ili kukimbia mifereji ya maji.<br>• Matengenezo ya mara kwa mara, na ukarabati wa haraka wa mfumo wa maji taka na mifereji ya maji.<br>• Mtetezi ataomba idhini kutoka kwa HOMAWASCO kwa ajili ya kuunganishwa kwenye bomba la maji taka la umma.<br>• Tengeneza Mpango wa Kudhibiti Utiririshaji wa Maji Taka (EDCP) kwa ajili ya uendeshaji wa mradi uliopendekezwa wakati wa awamu ya operesheni |
| Athari za trafiki | • Weka ishara za onyo/taarifa za kimkakati ili kuonyesha saa za kazi.<br>• Kuendeleza na kutekeleza mpango wa usimamizi wa trafiki.<br>• Hakikisha unafuatwa na sheria ndogo za trafiki za serikali ya Kaunti ya Homa Bay na sheria za trafiki za Kenya. |
| Uzalishaji wa taka ngumu. | • Kutoa mapipa ya kutenganisha na kurukwa kwa taka zinazozalishwa ili kuwezesha kuokoa, kuchakata tena, kutumia tena, na utupaji wa nyenzo / taka.<br>• Hakikisha kwamba maeneo ya kukusanya taka yanawekwa nadhifu, safi na yamewekwa alama wazi.<br>• Mkataba wa kidhibiti taka kilichosajiliwa na NEMA kukusanya na kutupa taka kwa wakati unaofaa katika tovuti zilizoteuliwa za NEMA.<br>• Wape wakazi mifuko ya taka ya plastiki iliyoidhinishwa na NEMA mara kwa mara |
| Kuongeza nishati matumizi na mahitaji. | • Ikiwezekana sakinisha na utumie nishati ya jua kwa taa za barabarani na eneo la kawaida.<br>• Ufungaji wa matumizi ya nishati<br>• Tengeneza dirisha kubwa kwa taa asilia na uingizaji hewa ili kupunguza nishati |
| Kuongezeka kwa mahitaji na matumizi ya maji. | • Kutoa matanki ya kuhifadhia maji iwapo usambazaji wa maji umekatizwa.<br>• Ikiwezekana fanya uvunaji wa maji ya paa.<br>• Kuweka utaratibu wa kugundua uvujaji kama vile ukaguzi wa mara kwa mara na matengenezo ya kawaida itasaidia kuokoa kiasi kikubwa cha maji.<br>• Vitengo vya makazi ya maendeleo vijazwe na uwekaji wa maji kwa ufanisi na usakinishaji. |

Ripoti kamili ya mradi unaopendekezwa inapatikana kwa ukaguzi wakati wa saa za kazi katika
:

1. **Katibu,**
   **Mizara ya Mazingira na Misitu,**
   **NHIF Building, 12th Floor,**
   **Ragati Road, Upper Hill,**
   **P.O.BOX: 30126-00100**
   **NAIROBI**

2. **Mkurugenzi Mkuu, NEMA**
   **Popo Road, off Mombasa Road,**
   **P.O. BOX 67839-00200,**
   **NAIROBI**

3. **County Director of Environment**
   **HOMA BAY COUNTY**

Nakala ya ripoti ya EIA inaweza kupakuliwa katika **www.nema.go.ke**

NEMA inawaalika wananchi kuwasilisha maoni ya mdomo au maandishi ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa notisi hii kwa Mkurugenzi Mkuu, NEMA, ili kusaidia Mamlaka katika mchakato wa kufanya maamuzi ya mradi huu. Tafadhali nukuu kumbukumbu. Namba **NEMA/EIA/5/2/2052.**
Maoni yanaweza pia kutumwa kwa barua pepe kwa **dgnema@nema.go.ke**

**MAMO B. MAMO, EBS**
**MKURUGENZI MKUU**

***Tangazo hili limefadhiliwa na mtetezi.***

# Wizara ya Ulinzi, US kufunza wafanyakazi raia wanaohudumu jeshini

**NA BOGITA ONGERI (PCO)**

Waziri wa Ulinzi Aden Duale amesisitiza kujitolea kwa Wizara yake kuwapa wafanyakazi raia wanaofanya kazi katika Wizara yake ujuzi unaofaa ili wafanye kazi yao vyema.

Akizungumza baada ya warsha ya siku tatu kati ya wakuu wa idara tofauti na maafisa kutoka Afisi ya Ushirikiano wa Kenya na Amerika (KUSLO), Waziri alisema sehemu ya raia wanaofanya kazi katika Wizara hutekeleza jukumu muhimu kusaidia jeshi kuzingatia jukumu lake la Kikatiba la kulinda na kukinga utukufu na Mipaka ya Jamhuri.Duale alisema kwamba kuna haja ya kupanua ufahamu wa raia hao katika juhudi za kuinua motisha wao kwa kuwawezesha kukuza kazi na kuzidumisha ili kuimarisha utendaji kazi wao. Ujumbe wa KUSLO uliongozwa na mwakilishi wa Taasisi ya Usimamizi wa Usalama, Bw Jessie Evans.

Waziri alishukuru ujumbe wa KUSLO kwa warsha hiyo ambayo ilitambua maeneo ya kupatiwa kipaumbele katika mafunzo ya raia kama vile Mkakati katika Uongozi, Maadili na Usimamizi, kusaidia shughuli za amani, ujuzi wa majadiliano na jukumu la usimamizi la raia katika vikosi vya ulinzi miongoni mwa mengine. Alisifu uhusiano mwema kati ya nchi hizi mbili ambao alisema umewezesha Jeshi la Ulinzi la Kenya (KDF) kuwa na mafunzo ya pamoja na Wanajeshi wa Amerika na akaongeza kuwa wakati umefika wa kuzingatia mipango ya mafunzo ya wafanyakazi raia ambayo itainua ujuzi wao.



**Waziri wa Ulinzi Aden Duale akipokea sarafu kutoka kwa mwakilishi wa KUSLO, Bi Jessie Evans.**

# Waziri ahakikishia wawekezaji katika Konza Technopolis usaidizi wa serikali

**NA JOSEPH NG'ANG'A (KNA)**

Waziri wa Habari Mawasiliano na Uchumi Dijitali) Eliud Owalo amehakikishia wawekezaji katika Konza Technopolis kwamba serikali imejitolea kutekeleza mradi wa Konza kama sehemu ya ajenda yake ya uchumi dijitali.

Serikali ya Kenya Kwanza inalenga kusaidia mradi huo kupitia Mswada wa Konza na kupatia wawekezaji motisha wa ushuru kwa nyenzo za ujenzi na ili kuharakisha miundomsingi ya mradi huo. Akisisitiza kuwa Konza Technopolis itaanza kutengeneza simu nafuu za mkono na programu za kompyuta hivi karibuni, Owalo alisema kwamba serikali tayari imewekeza pakubwa katika mradi huo na imejitolea kufanikisha mradi huo kwa viwango vya kimataifa.




**Waziri Eliud Owalo akihutubia kongamano la wawekezaji la kila mwaka katika Konza Technopolis.**

Akizungumza katika kongamano la kila mwaka la Wawekezaji katika at Konza Technopolis, Owalo alisema: "Uwepo wangu hapa leo ni kuwahakikishia kwamba serikali imejitolea kutekeleza Konza Technopolis kuwa Jiji la kiwango cha ulimwengu. Wizara yangu inatia bidii kuhakikisha tunatayarisha Mswada wa Konza ili kuweka mradi huu katika sheria kulinda maslahi ya wawekezaji wetu."

"Tumewekeza pakubwa katika Konza na tutaendelea kusaidia taasisi hiyo kutekeleza jukumu lake. Tunafurahia hatua ambazo jiji hili limepiga ikiwemo kuanzishwa kwa Taasisi ya Mafunzo ya Juu ya Sayansi na Tekinolojia Kenya (KAIST) ambayo inajengwa kwa ushirikiano wa Wizara ya Elimu," alisema Owalo.

KAIST inatarajiwa kusajili wanafunzi wake wa kwanza kufikia mwisho wa mwaka huu. Ujenzi wa taasisi hiyo tayari unaendelea katika jiji hilo.

Akihimiza wawekezaji hao kuhamishia biashara zao Konza, waziri alisema kwamba serikali iko tayari kutatua changamoto ambazo huenda wakapata katika kuendeleza biashara zao. "Katika kiwango cha sera, tunapatikana kuhakikisha tuko na sera zinazofaa kwa jiji hilo. Tutahakikisha kwa mtazamo wa sera kuna sera za kutosha, sheria na kanuni zitakazowezesha uwekezaji wa sekta ya kibinafsi ndani ya Konza," asema.

> Tumewekeza pakubwa katika Konza na tutaendelea kuinga mkono- Waziri Owalo

Katika hafla hiyo ambayo ilihudhuriwa na Katibu wa ICT na Uchumi Dijitali Mhandisi John Tanui, Kaimu Afisa Mkuu Mtendaji w KoTDA, Bw John Paul Okwiri alisema wanatarajia wawekezaji wapatao watano kuanza kujenga Konza katika miezi 12 ijayo.

" Tunafurahia uwekezaji ambao tumefanya kama jiji. Kuendelea mbele tunataka kuharakisha ujenzi wa miundomsingi . Katika miezi 12 ijayo tunatarajia wawekezaji wasiopungua watano wakianza shughuli za ujenzi wa majengo," alisema.

Kufikia sasa, wawekezaji 25 katika awamu ya kwanza wamepata ardhi na ikasajiliwa huku miundo ya wawekezaji kumi ikiwa imeidhinishwa.

NCA
NATIONAL CONSTRUCTION AUTHORITY

## NOTISI YA TENDA WAZI YA KITAIFA

